
Mafunzo ya Ufugaji



MKL
SF489
.K8

# Kufuga na Kuboresha Kuku wa Kienyeji

INADES - Formation Tanzania

# Mafunzo ya Ufugaji

SNAL - SUA / O
057410 3

# Kufuga

# na

# Kuboresha Kuku wa Kienyeji

SOKOINE UNIVERSITY LIBRARY
20/09/18

INADES - Formation Tanzania
S.L.P. 203 Dodoma
Simu:061/354230 Fax 061/354722
Email:INADES-FO@maf.org

Tunatoa shukrani za dhati kwa shirika la "Cooperation in Development" (CODEL)
ambalo lilitoa msaada ili kijitabu hiki kichapishwe

© 1992 INADES - Formation Tanzania
Ni marufuku kunakili, kutafsiri au kuyatoa yaliyomo katika kitabu hiki, kwa njia yoyote, katika nchi yoyote, bila idhini iliyoandikwa kutoka INADES - Formation Tanzania

# Kufuga na Kuboresha Kuku wa Kienyeji

## Mpango wa Kitabu


| | Ukurasa |
| --- | --- |
| **Utangulizi** | 5 |
| **Sehemu ya Kwanza:** | |
| **AINA ZA KUKU** | 7 |
| Kuku wa kienyeji | 7 |
| Kuku wa Kigeni | 11 |
| Koo za kuku wa mayai | 11 |
| Koo za kuku wa nyama | 12 |
| Koo za kuku wanaotoa mayai na nyama | 13 |
| Jinsi ya kuwapata kuku wa kigeni | 15 |
| **Sehemu ya Pili:** | |
| **KUBORESHA KUKU WA KIENYEJI** | |
| Kulea vifaranga chotara kizazi cha kwanza | |
| Kuku chotara kizazi cha pili | |
| Lishe ya kuku walioboreshwa | |
| **Sehemu ya Tatu:** | |
| **NJIA MBALIMBALI ZA KUFUGA KUKU** | |
| Sifa za banda bora la kuku | 33 |
| Kufuga nusu ndani - nusu nje | 35 |
| Kufuga ndani ya banda tu | 37 |
| Hifadhi ya kuku ndani ya banda | 38 |
| Vifaa ndani ya banda | 38 |
| Usafi ndani ya banda | 42 |
| Kuokota mayai | 42 |
| Njia nzuri ya kumbeba kuku | 43 |

**Sehemu ya Nne:**
**MAGONJWA YA KUKU** 45
Dalili na Jinsi ya Kudhibiti 45
Dalili za jumla za magonjwa ya kuku 46
Muhtasari wa magonjwa na jinsi ya kuyadhibiti 47
Muhtsari wa wadudu muhimu wanaoshambulia kuku 49

**Sehemu ya Tano:**
**KUSIMAMIA UFUGAJI WAKO** 51
Kutunza kumbukumbu za ufugaji wa kuku 51
Kumbukumbu za kuku wa nyama 52
Kumbukumbu za kuku wa mayai 53
Jinsi ya kufahamu faida unayopata 53

**Neno la mwisho** 55
**Tukumbuke maneno haya** 57

# Utangulizi

Tanzania ina idadi kubwa ya kuku wa kienyeji
wanaofugwa kwa mtindo wa huria
vijijini na hata mijini.
Katika mtindo huu wa ufugaji,
kuku huachwa huru mchana kutwa
kujitafutia chakula wao wenyewe.

Pengine baadhi ya wakulima
huwatupia kuku wao mabaki ya chakula,
chenga za nafaka au nafaka zenyewe.
Wapo pia wakulima walio na utaratibu
wa kuwapa kuku wao
pumba za nafaka na maji ya kunywa
kila inapowezekana.

Zinapofika nyakati za jioni
kuku hulala jikoni,
au ndani ya nyumba ya mkulima mwenyewe.
Ingawaje ufugaji wa aina hii ni rahisi, lakini faida inayopaikana
(kama ipo) ni ndogo sana.

Kutokana na kuzaana wenyewe wa wenyewe
(kutobadili jogoo),
lishe duni n.k.,
kuku hawa wana umbo dogo.
Hutaga mayai machache, tena madogo madogo.
Nyama yao ina ladha nzuri,
lakini kwa vile wana umbo dogo,
kiasi cha nyama wanayotoa ni kidogo tu.

Katika kijitabu hiki
“**Kufuga na Kuboresha Kuku wa Kienyeji**”
tutazungumzia jinsi ya kuboresha kuku wa kienyeji
kwa njia ya uzalishaji,
kutumia jogoo bora,
kuboresha lishe ya kuku.

Tutazungumzia pia njia mbalimbali za kufuga
zinazoweza kumnufaisha mfugaji mdogo.

Kutokana na maarifa haya
wewe mkulima utaweza kuona haja
ya kufanya mabadiliko katika ufugaji wako.
Ili uweze kunufaika na ufugaji
ni lazima uwe na mifugo bora.

Kitabu hiki kimeandikwa
ili kukupatia maarifa na mbinu za kutumia
ili upate kuku bora
kutokana na kuku wako wa kienyeji.

Katika kitabu kingine “ Kufuga kuku wa biashara”
Utajifunza maarifa na mbinu bora
za ufugaji wa kuku wa biashara.
Hawa ni kuku wa kigeni.
Wanahitaji matunzo maalum tofauti
na yale ya kuku wa kienyeji wanaoboreshwa.

## Sehemu ya Kwanza

# AINA ZA KUKU

Kuna aina kuu mbili za kuku
wanaopatikana hapa nchini.
Kuku wa **kienyeji** na kuku wa **kigeni.**

Kuku wa kienyeji wana umbo dogo.
Hutaga mayai machache na madogo madogo;
pia wana nyama kidogo tu.

Kuku wa kigeni wanaweza kuwa
kuku wa mayai,
kuku wa nyama
na kuku wanaotoa mayai na nyama
katika viwango vya kuridhisha.
Aina zote tatu za kuku wa kigeni
zina umbo kubwa ukizilinganisha na kuku wa kienyeji.

## Kuku wa Kienyeji

Ndani ya kundi la kuku wa kienyeji
zipo aina kadhaa za kuku.
Asili ya kuku hawa
ni **kuzaliana** kwa muda mrefu
kwa kuku wepesi (wadogo wadogo) wao kwa wao.


Pamoja na sifa tulizozitaja hapo juu,
kuku hawa wana uwezo wa kuhimili mazingira magumu,
kuatamia mayai mpaka kutotoa vifaranga,
kulea vifaranga
na hata kujitafutia chakula wao wenyewe.


Siyo rahisi kuainisha aina za kuku wa kienyeji. Hata hivyo, pengine kuku hawa huweza kuainishwa kutokana na umbo la mwili.

* Wengine

wana

miguu mifupi.






* Wengine

wana

miguu mirefu.

Njia nyingine ya kuainisha kuku wa kienyeji ni kwa kuangalia manyoya yao.




* Wengine

huwa

hawana

manyoya shingoni.



* Wengine

wana

Manyoya

yaliyosimama


mwili mzima.

* Wengine

hawana

manyoya

mkiani.



**Sifa nzuri za kuku wa kienyeji**

- Wanahimili baadhi ya magonjwa yanayowaua kuku wa kigeni.
- Wanakula kiasi kidogo cha chakula.
- Wana uwezo mkubwa wa kuatamia mayai, kutotoa na kulea vifaranga.
- Wanatoa mayai na nyama yenye ladha nzuri.

**Kasoro za kuku wa kienyeji**

- Hawatagi mayai mengi.
- Mayai yao huwa madogo madogo.
- Wanatoa kiasi kidogo tu cha nyama.
- Wanatumia muda mwingi kuatamia mayai na kulea vifaranga;
  hivyo kufanya kipindi chao cha kutaga kuwa kifupi katika maisha yao.

# Kuku wa Kigeni

Hawa ni kuku ambao asili yao ni nchi za nje.
Kuku wa kigeni wanaofugwa hapa Tanzania
waliingizwa kutoka nchi za Ulaya na Marekani.
Wengi wao hutoa mazao (mayai na nyama)
kwa wingi kuliko kuku wa kienyeji.
Kila kundi la kuku wa kigeni
lina aina kadha za kuku.
Aina ya kuku kwa urahisi tutaiita ukoo wa kuku.

## Koo za Kuku wa Mayai


Hizi ndizo koo za kuku zinazojulikana
kwa utagaji wa mayai kwa uwingi.
Kuku hawa hutumia sehemu kubwa ya chakula chao
kwa kutengeneza mayai ndani ya miili yao.

*White leghorn*

Hawa ni kuku wepesi.


Wana rangi nyeupe.

Pia wao hutaga mayai meupe.



Kuku wa ukoo wa ***White leghorn***

*Rhode island red*
Hawa ni kuku wazito kuliko *white leghorn.*
Wana rangi nyekundu,
na hutaga mayai ya rangi ya kahawia.



Kuku

wa

ukoo

wa

***Rhode island red.***


Koo nyingine za kuku wa mayai
ni ***Black Australorp*** ambao ni weusi mwili mzima,
na ***New Hampshire*** ambao ni wekundu.

**Koo za Kuku wa Nyama**

Hizi ndizo koo za kuku wa nyama zinazojulikana
kutokana na uwezo wake mkubwa wa kutoa nyama.
Kuku hawa hutumia sehemu kubwa ya chakula wanachokula
kwa kutengeneza nyama nyingi mwilini.

***Hypeco***

Hawa ni kuku weupe wenye uwezo wa kukua upesi,
na hivyo kutoa nyama nyingi katika kipindi kifupi
tangu kifaranga kutotolewa.



Kuku


wa ukoo

wa *Hypeco*

Koo nyigine za kuku wa nyama ni **Hubbard** na **Lohman.**


**Koo za Kuku Wanaotoa Mayai na Nyama**

Koo maarufu zinazojulikana kwa sifa hizi
ni ***Plymouth Rock.***
Ni kuku wazito.
Wana rangi nyeupe na mabaka mekundu.



Kuku
wa
ukoo
wa
***Plymouth Rock***

***Light sussex***
Hawa wana rangi nyeupe na madoadoa meusi.



Kuku
wa
ukoo
wa
***Light sussex***

Koo zote tulizozitaja hapo juu
zina kuku asili.
Kila ukoo kuku wake wamezalishwa
kwa kutumia majogoo na makoo
kutoka katika ukoo huo tu.

Aina nyingine za kuku ni **machotara** (hybrids)
wanaozalishwa kutokana na koo mbili tofauti.
Mfano wa kuku aina ya machotara ni
***Shaver, Warren, Arbo, Acre na Thormber.***

**Ubora wa kuku wa kigeni**

- Kuku wa mayai hutaga mayai mengi.
- Kuku wa nyama hutoa nyama nyingi
  kuliko kuku wa kienyeji.

## Kasoro za Kuku wa Kigeni

- Hawahimili magonjwa kama kuku wa kienyeji.
- Huhitaji chakula kingi kuliko kuku wa kienyeji.
- Huhitaji matunzo maalum (ndani ya banda).
- Hawana tabia ya kuatamia mayai
  na kutotoa vifaranga.

## Jinsi ya Kuwapata Kuku wa Kigeni

Hapa nchini kuku wa mayai au wa nyama
hupatikana katika vituo maalum
vya kutotoa vifaranga.
Baadhi ya vituo hivi hundeshwa na serikali,
mashirika na makampuni mbalimbali
na hata watu binafsi.

Vituo vinavyojulikana
kwa ajili ya kutoa huduma hii ni:

Ukonga - Dar es Salaam
Interchick - Kijenge (Arusha)
Shirika la Kilimo Uyole - Mkoa wa Mbeya
Shirika la Elimu Kibaha - Mkoa wa Pwani
Kiwanda cha Magogo Mpwapwa - Mkoa wa Dodoma
Kilacha - Mkoa wa Kilimanjaro
Makoko Seminary - Musoma, Mkoa wa Mara.

Kutegemea na mahali ulipo,
**kama unataka kuanza kufuga**
au kuboresha ufugaji wako wa kuku,
omba ushauri wa mtaalam wa mifugo wa eneo lako.
Yeye atakuelekeza mahali
**utakapopata majogoo**
wanaofaa kufuatana na mahitaji yako.

Katika sehemu hii ya kijitabu
umejifunza aina mbalimbali za kuku wa kienyeji.
Umeona pia kuwa kuku hao ni wavumilivu;
lakini hutoa faida ndogo tu kwako.

Umejifunza pia koo mbalimbali za kuku wa kigeni.
Kuku hao hutoa mazao mengi,
hivyo wanaweza kukupatia faida kubwa.
Kwa kuwa kuku wa kigeni
siyo wavumilivu kama wale wa kienyeji
ufugaji wao huhitaji uangalifu mkubwa.

Katika sehemu ya pili ya kitabu hiki
utajifunza jinsi ya kuboresha kuku wa kienyeji
kwa kutumia majogoo wa kuku wa kigeni.

## Sehemu ya Pili

# KUBORESHA KUKU WA KIENYEJI

Wewe mkulima unahitaji mayai na nyama ya kuku
kwa ajili ya lishe ya familia yako.
Pia unahitaji mayai na kuku wa ziada
ambao utawauza na kujipatia pesa
kwa ajili ya matumizi mbalimbali.
Ni rahisi kulifikia lengo hili
kama utafuga kuku wa kigeni.

Lakini kutokana na kasoro walizo nazo kuku wa kigeni,
ni wazi kuwa ufugaji wao unahitaji gharama kubwa
na uangalifu mkubwa.
siyo kila mkulima anaweza kuumudu.

Njia nafuu ya kulifikia lengo la kujitosheleza
kwa mayai na nyama ya kuku,
ni kwa **kuboresha kuku wa kienyeji** hatua kwa hatua.
Hii unaweza kufanya **kwa kutumia majogoo wa kigeni**
kwa kufuata utaratibu ufuatao.

**Hatua za Kwanza**


- **Chagua makoo** yenye uzito mkubwa,
  yenye afya nzuri
  na yanayohimili magonjwa ya kawaida ya hapo ulipo.

- Chinja ule, au uza
  majogoo **yote** yaliyopo.

- Nunua au **jipatie jogoo bora**
  wa ukoo wa nyama na mayai

kwa mfano *Light sussex*,
*Plymouth Rock* au *Thormber*
Aina hizi za majogoo unaweza kuzipata
kutoka kituo cha utotoaji vifaranga
kilicho jirani na hapo ulipo.
Omba ushauri wa mtaalam wa mifugo wa eneo lako
kabla hujaleta jogoo
ili akushauri ni jogoo wa ukoo upi atafaa,
na jinsi ya kumtunza.

Baada ya kupata idadi ya majogoo bora unayotaka,
waweke pamoja na makoo
katika uwiano wa jogoo mmoja kwa makoo 10 - 15



Jogoo bora


## Kulea Vifaranga Chotara Kizazi cha Kwanza

Baada ya jogoo wa kigeni
kumpanda koo wa kienyeji,
koo atataga mayai
na kutotoa vifaranga chotara kizazi cha kwanza.

Vifaranga hivi vinarithi nusu kutoka kwa baba yao
na vinarithi nusu kutoka kwa mama yao.

Kutoka kwa mama yao (koo wa kienyeji)
vinarithi **uwezo wa kuhimili magonjwa**
na kuvumilia hali ngumu ya mazingira
(hasa joto, baridi).

Kutoka kwa baba yao (jogoo bora wa kigeni)
vitakuwa na **mwili mkubwa** kuliko kwa mama yao.
Vitatoa **mayai mengi**
na **nyama nyingi** kuliko mama yao



Koo la kienyeji
na vifaranga vyake
wa kizazi cha kwanza

Baada ya vifaranga chotara kutotolewa
waache na mama yao katika chumba safi
kwa muda wa mwezi mmoja.

## JINSI YA KUBORESHA CHAKULA CHA VIFARANGA

Ili kifaranga awe na afya nzuri na akue upesi anahitaji chakula maalum.
Chakula hicho ni mchanganyiko wa viini lishe mbalimbali.
Kila kiini lishe ni lazima kiwe katika kiwango sahihi kulingana na mahitaji ya mwili wa kifaranga.
Viini lishe anavyohitaji kifaranga ni:

- Wanga
- Mafuta
- Protini
- Vitamini
- Madini
- Maji

Mchanganyiko sahihi wa viini lishe kwa mahitaji ya kifaranga, humwezesha kukarabati na kujenga (kukua) mwili haraka.

## JINSI YA KUVIPATA VIINI LISHE

Viini lishe tulivyovitaja hapa juu hupatikana katika aina mbalimbali za viungo ghafi vya chakula cha vifaranga kama ifuatavyo.

**Wanga**
Wanga hupatikana katika pumba, chenga au dona ya nafaka kama mahindi au matama aina ya serena, lulu n.k.

**Mafuta**
Mafuta hupatikana katika mbegu kama karanga au alizeti.
Mbegu hizi zikikamuliwa mashudu yake hubaki na kiasi fulani cha mafuta.

**Protini**
Kiini lishe hiki hupatikana
katika mashudu ya karanga au alizeti,
damu ya wanyama kama ng'ombe, mbuzi n.k.

Damu hiyo unaweza kuipata machinjioni.
Changanya damu mbichi na pumba katika ndoo
au chombo chochote kilicho wazi upande mmoja.
Vuruga mchanganyiko huo kwa kipande cha mti,
halafu fikicha kwa viganja ili kuondoa mabonge.
Sambaza mchanganyiko huu juu ya bati
halafu anika juani mpaka ukauke kikamilifu.

Protini hupatikana pia katika unga wa mbegu
za jamii ya kunde kama maharage, kunde, soya n.k.

**Madini**
Madini aina ya 'Calcium' (tamka kalshium)
na fosforasi hupatikana katika unga wa dagaa.

**Vitamini**
Vitamini hupatikana katika majani mabichi
ya mti aina ya Lusina,
majani ya mpapai,
mchicha wa nyumbani au wa porini.

Vitamini hupatikana pia
katika majani ya mimea ya jamii ya mikunde
kama marejea na luseni.
Unaweza kukausha mimea hiyo
na kuponda katika kinu
au kufikicha kwa viganja ili kupata unga.

Viungo ghafi tulivyovitaja hapo juu huwa vinapatikana katika vijiji vingi hapa nchini. Kwa hiyo wewe mkulima **unaweza kujitengenezea mwenyewe chakula kinachofaa kwa ajili ya vifaranga wako.**


075 4103

**Kuwatengenezea Chakula Vifaranga Wenye Umri wa Siku 1 Mpaka Miezi Miwili**

**Matayarisho:**

- Andaa aina zote za viungo ghafi zilizo bora katika viwango vya kutosha.
  Pumba au dona, mashudu n.k. viwe havikuvunda.
  Tena viwe safi yaani havikuchanganyika na uchafu wowote, au kushambuliwa na wadudu.

- Tayarisha kopo tupu lenye ujazo wa lita 1 sawa na uzito wa kilo 1.
  Mfano wa kopo linalofaa ni lile la **Tan Bond, Pride, Kimbo** au **Blue band.**




Haya ndiyo mahitaji yako (viungo ghafi) kabla ya kuchanganya chakula cha vifaranga.

## Kuchanganya Chakula cha Vifaranga

Kifaranga anapokuwa katika umri
wa miezi miwili ya kwanza
huhitaji protini kwa wingi aweze kujenga mwili.
Ili upate chakula kilichochanganyika kikamilifu
ni muhimu uvitenge viungo ghafi katika mafungu mawili.

**Kwanza** pima kwa kopo
halafu changanya viungo ghafi vyote
vyenye uzito mkubwa katika fungu lake.
Kwa mfano:

Pumba za mahindi
Dona ya mahindi au serena
Unga wa maharage na
Mashudu ya alizeti.

Katika **fungu la pili** pima halafu changanya:

Unga wa dagaa
Unga wa majani ya Lusina au Luseni na chumvi.

Mwisho changanya mafungu yote mawili kikamilifu.

### Viwango vya Kuchanganya


**Fungu la kwanza** (Viungo ghafi vizito)

| **Kiungo ghafi** | **Kiwango/Makopo ya kilo 1** |
|---|---|
| Pumba za mahindi | 26.0 |
| Dona ya mahindi au serena | 35.0 |
| Unga wa maharage | 15.0 |
| Mashudu ya alizeti au damu iliyokaushwa | 6.0 |

**Fungu la pili** (Viungo ghafi vyepesi)

| | |
|---|---|
| Unga wa dagaa | 7.5 |
| Unga wa majani ya Lusina au Luseni | 10.0 |
| Chumvi ya jikoni | 0.5 |
| Jumla ya Makopo | 100.0 |

Kama kiasi cha chakula ni kingi changanya kwa koleo.
Kama kiasi ni kidogo tu changanya kwa mikono.



Kuchanganya chakula kingi kwa koleo

Ukitaka kuchanganya chakula chenye jumla ya makopo 50 pima nusu tu ya kiwango cha kila kiungo ghafi kilichoonyeshwa katika jedwali hapo juu.


Kwa mfano badala ya kupima makopo 26 ya pumba pima makopo 13 ...
Badala ya makopo 35 ya dona, pima makopo 17.5, n.k.

Ukitaka kuchanganya chakula
chenye jumla ya makopo 25 au debe 1
pima **robo** tu ya kiwango cha kila kiungo ghafi
kilichoonyeshwa hapo juu.

Ili ufanikiwe kuwatengenezea vifaranga wako
chakula cha mchanganyiko
ni muhimu ujiandae mapema.
Tafuta mahitaji yako yote
na kuyahifadhi vizuri
kabla vifaranga havijatotolewa.


## Kulisha Vifaranga

Ili chakula hiki kisiharibiwe na mama yao
watenganishe vifaranga na mama yao
walau kwa muda wa mchana tu.
Halafu weka chakula katika vilishio
na kuwapatia vifaranga wako.
Pia wawekee maji safi
na ya kutosha ya kunywa wakati wote.
Jioni mrudishe mama yao
ili awakinge vifaranga dhidi ya baridi
wakati wa usiku.



Kuku anawakinga vifaranga dhidi ya baridi

Njia nyingine ya kulea vifaranga
ni kuwatenganisha na mama zao
mara baada ya kutotolewa.
Watunze vifaranga ndani ya kitalu
kilichotengenezwa kwa mbao
au karatasi ngumu zinazotumika kujengea dari.
Weka taa ndani ya kitalu
ili kuwapa joto vifaranga.



Vifaranga vikiwa ndani ya kitalu

Mrudishe koo aliyetenganishwa na vifaranga
katika kundi lenye jogoo mara moja.
Atapandwa na kuanza kutaga mayai tena
baada ya muda mfupi.

Kwa kufuata utaratibu huu
utajipatia vifaranga chotara vya kizazi cha kwanza
kwa wingi,
na kwa gharama nafuu.

Wapatie vifaranga **dawa za kinga**
dhidi ya magonjwa kama **kideri** au **mdondo**.
Omba ushari kwa mataalam wa mifugo
akuelekeze jinsi ya kutekeleza kwa vitendo maarifa haya.

Katika sehemu ya nne ya kitabu hiki
tunazungumzia baadhi ya magonjwa ya kuku
ambayo hutokea mara kwa mara.
Pia tunazungumzia tiba na kinga zake.

**Kutengeneza Chakula cha Vifaranga Wanaokua**
(Wenye Umri wa Miezi Miwili)

Vifaranga wakifikisha umri wa miezi miwili
huhitaji chakula chenye wanga mwingi
kuliko hapo awali.
Wanga huwapatia nguvu na joto mwilini.
wakiwa na nguvu ya kutosha
vifaranga watakula vizuri chakula unachowapatia,
hivyo wataendelea kuwa na afya nzuri
na kukua upesi.
Ili kuwawezesha kupata mahitaji haya,
kwa kufuata utaratibu ule wa kwanza
changanya chakula chao kama ifuatavyo.

| **Aina ya Kiungo ghafi** | **Kiwango/makopo ya kilo 1** |
|---|---|
| Pumba za mahindi | 44.0 |
| Dona ya mahindi au serena | 30.0 |
| Unga wa dagaa | 5.0 |
| Unga wa maharage au kunde | 15.0 |
| Majani ya Lusina au Luseni makavu yaliyotwanga | 5.0 |
| Chokaa | 0.5 |
| Chumvi ya jikoni | 0.5 |
| Jumla ya makopo | 100.0 |

Pamoja na chakula hiki
wapatie **maji mengi na safi** ya kunywa.
Pia wape **majani mabichi** ya mipapai,
marejea au mchicha wa porini.
Majani haya yana vitamin A na C ndani yake.
Kuku wanahitaji sana vitamini hizi.

## Kutenganisha Majogoo na Tembe

**Tenganisha majogoo na tembe**
wanapokaribia kupevuka (miezi 3 - 4).
Hatua hii itakuwezesha kuepuka uwezekano wa kuku
wenye uhusiano wa damu kupandana wenyewe kwa wenyewe.

**Ili makoo chotara wasipandwe na baba yao**
(jogoo wa kwanza) mchinje na kumla
au muuze au badilishana na mtu mwingine.
**Mweke jogoo mwingine** ambaye
hana uhusiano na makoo yote.
**Badilisha jogoo kila baada ya mwaka mmoja.**

## Kuku Chotara Kizazi cha Pili


**Makoo chotara wa kizazi cha kwanza**
**wakipandwa na jogoo bora**
watataga mayai makubwa na mengi.
Watatotoa vifaranga vikubwa,
ndio **chotara wa kizazi cha pili.**
Vifaranga hivi vitakuwa na asilimia 75
ya damu ya kigeni.

Vitafanana zaidi na kuku bora kitabia
na katika uwezo wa kuzalisha zaidi mazao yao.
Yaani kuku chotara wa kizazi cha pili
watatoa mayai ya nyama kwa uwingi zaidi
kuliko kuku chotara wa kizazi cha kwanza.

kwa hali hiyo vifaranga chotara vya kizazi cha pili
**vinahitaji matunzo bora zaidi**
kuliko kuku wa kienyeji.
Matunzo haya ni pamoja na kuwajengea banda bora,
kuwapatia lishe bora,
na kuwapatia kinga na matibabu
dhidi ya magonjwa na vimelea mbalimbali.

Kuku machotara wa kizazi hiki
ndio watakaokufaa
kwa utagaji wa mayai na utoaji wa nyama.

**Hawa ndio kuku walioboreshwa.**



## Lishe ya Kuku Walioboreshwa

Kuku chotara wa kizazi cha pili
watataga mayai vizuri kama unawalisha vema.

Ili kuku atage yai
anahitaji chakula aina ya wanga.
Hiki humpa nguvu na joto mwilini.

Pia anahitaji protini.
Hizi hutumika katika kujenga au kukarabati sehemu za mwili zilizoathiriwa na kufanya sana kazi au na maradhi.

Kadhalika na madini kama chumvi na chokaa; maji, majani mabichi na aina nyingine za vyakula. Vyote hivi kila kimoja kina kazi maalum katika mwili wa kuku.

Kwa hiyo ili kuku atage mayai kwa wingi na abaki na afya nzuri, anahitaji kupatiwa chakula kinachompatia mahitaji yake yote ya mwilini, na cha ziada kwa kutengeneza mayai.

Unaweza kutengeneza chakula cha aina hii wewe mwenyewe kwa kutumia mchanganyiko ufuatao.

Fuata utaratibu ule ule tulioeleza hapo awali (uk. 23.) wakati wa kuchanganya chakula cha vifaranga wakiwa katika mwezi wao wa kwanza.

| | Kiwango/Makopo ya Kilo 1 |
|---|---|
| Pumba za mahindi | 19.8 |
| Dona ya serena | 49.0 |
| Mashudu ya alizeti | 3.0 |
| Lusina (majani makavu) | 5.0 |
| Dagaa | 11.0 |
| Chokaa na jivu | 11.9 |
| Madini | 0.3 |
| Jumla | 100.0 |

**Madini** hupatikana katika maduka ya dawa za mifugo.
Hivyo omba ushauri wa mtaalamu wa mifugo
aliye jirani na hapo ulipo
akuelekeze jinsi ya kupata madini hayo.

Pamoja na chakula hiki,
kuku wa mayai anahitaji **maji safi** ya kunywa
na ya kutosha.

Pia mpatie **majani mabichi**
kama ya mpapai, marejea, Lusina
na mchicha wa porini.
Majani haya yana vitamini A na C.
Kuku wanaotaga wanahitaji sana vitamini hizi.

Majani mabichi pia yana viini vinavyoitwa
"*carotine*" (tamka karotini).
Viini hivi ndivyo vinavyofanya
sehemu ya katikati ya yai
kuwa na rangi ya njano.
Yai lenye kiini cha rangi ya njano
huvutia walaji.

Kuku wasiopewa majani mabichi mara kwa mara,
hutaga mayai yenye viini vya rangi ya kijivu.
Mayai ya aina hii hayavutii walaji.

Kuku wa kienyeji hutaga mayai
yenye kiini cha rangi ya njano wakati wote.
Hii hutokea kwa sababu kuku hao wapo huru nje
kujitafutia chakula chao,
ambacho ni pamoja na majani mabichi.

Katika sehemu hii ya kitabu,
umejifunza njia mbili za kulea vifaranga.
Pia umejifunza lishe bora ya vifaranga
wakiwa katika hatua mbalimbali za kukua.
Mwisho umejifunza lishe ya kuku walioboreshwa.

Jambo muhimu jingine ulilojifunza
ni kuwa sehemu kubwa ya viungo ghafi
vya chakula cha kuku
hupatikana vijijini mwetu.
Hivyo unayo nafasi kubwa
ya kujitengenezea wewe mwenyewe,
michanganyiko mbalimbali
ya chakula cha kuku wako.

Ukifanya kwa uangalifu kazi hii
utanufaika na matokeo yake.

Katika sehemu ya kitabu ifuatayo
utajifunza njia mbali mbali za kufuga kuku.

# Sehemu ya Tatu

## NJIA MBALI MBALI ZA KUFUGA KUKU

Kuna njia au mitindo mbalimbali ya kufuga kuku. Mambo yanayomfanya mkulima kuamua atumie mtindo fulani wa ufugaji ni pamoja na:

- Hali ya hewa ya mahali alipo
- Nia ya kufuga kuku hao
- Uwezo wa kugharamia shughuli za ufugaji wa kuku, n.k.

Katika sehemu hii ya kitabu utajifunza sifa za banda bora la kuku, na njia mbili tu za kufuga kuku:
kufuga nusu ndani - nusu nje,
na kufuga ndani tu.

### Sifa za Banda Bora la Kuku

Banda linalofaa kufugia kuku linatakiwa kuwa na sifa zifuatazo.

– **Liwe jengo imara.**
Pasiwe na sehemu zilizo wazi kwenye msingi au kati ya kuta na paa. Banda lijengwe kwa vifaa vinavyopatikana katika mazingira yako ili liwe la gharama nafuu. Jengo imara litazuia panya, vicheche, paka na nyoka kuingia ndani ya banda na kuwashambulia kuku.

- **Liwe rahisi kusafisha.**

Kuta na sakafu zisiwe na mipasuko.
Ni rahisi kuosha na kusafisha sakafu iliyo katika hali hii.
Sakafu au kuta zilizopasuka pasuka huficha wadudu kama viroboto, papasi n.k.

- **Pawe na usafi wa kudumu kuzunguka eneo la banda.**

Hali ya usafi itafanya wadudu kama siafu au mchwa, na wanyama kama panya na paka mwitu wakose maficho.

- **Liwe na nafasi ya kutosha kuku waliopo.**

Kwa kawaida eneo la mita 1 mraba (**sq.m.1**) au futi 3 mraba hutosha kufugia kuku 4 wanaotaga au kuku 8 wa nyama.

- **Liweze kuingiza hewa na mwanga wa kutosha.**

Banda lenye uwezo wa kuingiza hewa safi na kutoka ndani yake hubaki kavu.
Harufu mbaya zitatoka, hivyo kuwawezesha kuku kupumua hewa safi.

- **Lisiwe na joto sana au baridi sana.**


Panda miti kama Lusina kuzunguka banda, ili eneo liwe na kivuli cha kutosha na bila upepo mkali.

Banda la aina hii
litakuwezesha kudhibiti
kuenea kwa magonjwa mbalimbali
katika kundi lako.

# Kufuga Nusu Ndani - Nusu Nje

Huu ni mtindo wa kufuga ambapo
kuku wanaweza kushinda mchana
ama wakiwa ndani ya banda
au ndani ya ua.

**Aina ya banda** lifaalo kutumiwa
katika ufugaji huu
ni lile linalozungukwa na ua,
au lililounganishwa
na ua mbele yake.



Banda lililounganishwa na ua

Wakati wa mchana
kuku wapo huru
ama kushinda ndani ya banda,
hasa wanapotaka kutaga mayai,
au ndani ya ua.

## Faida za Kufuga Nusu Ndani - Nusu Nje

- Kuku watakuwa salama kutokana na maadui mbalimbali.
- Utaweza kuwalisha kuku wako vizuri hivyo wataongeza utoaji wa mazao yaani mayai na nyama.
- Itakuwa rahisi kwako kudhibiti wadudu na vimelea vinavyoleta magonjwa kwa kuku wako.
- Kuku watapata mwanga wa jua wa kutosha na hewa safi. Wakati wa joto (jua) kali watakuwa huru kuingia ndani ya banda na kukaa kivulini.
- Kuku hawataharibu mazao yako shambani au bustanini.
- Wewe mkulima utapata urahisi wa kukusanya mbolea na kuipeleka shambani.

## Hasara za Kufuga Nusu Ndani - Nusu Nje

Unahitaji kuwa na muda wa kutosha kwa ajili ya kuwahudumia kuku wako.

Hata hivyo, gharama za muda huo na za vifaa vingine zitafidiwa na mapato ya mradi kama utafuga kwa kufuata maarifa haya kwa vitendo.



Mkulima anayenufaika
na ufugaji wa kuku walioboreshwa

## Kufuga Ndani ya Banda Tu

Njia nyingine ya ufugaji wa kuku
inayotumika sana ukiondoa ufugaji huria
ni kufuga ndani.
Katika mtindo huu wa kufuga,
kuku huishi ndani ya banda maisha yao yote.

Kuku chotara wa kizazi cha pili na cha tatu
au kuku wa kigeni,
ndio wanaofaa kufugwa kwa njia hii.
Kwa ujumla wafugaji wa kibiashara walio wengi
hutumia njia hii ya kufuga.

Inaonekana gharama za ufugaji kwa njia hii ni kubwa, lakini huweza kufidiwa na mapato yanayotokana na kuku wenyewe.

Jambo muhimu kwako, ni kuwa na muda wa kutosha mchana kutwa ili kuwahudumia kuku kikamilifu.

**Hifadhi ya Kuku Ndani ya Banda**

Kwa sababu kuku wataishi daima ndani ya banda ni muhimu kujenga banda lenye sifa zote za ubora kama tulivyoona hapo awali. (uk. 33)


**Tandaza takakata za mbao sakafuni.**
Kazi ya takataka hizi nikunyonya unyevu wote unaotokana na kinyesi cha kuku.
Kama kutakuwa na takataka za kutosha sakafuni,
banda litakuwa kavu daima
na bila harufu mbaya
wala wadudu kama inzi.

Kuku na mayai huwa safi daima.
Kwa kutumia mtindo huu,
unaweza kufuga kuku wengi uwezavyo
kutegemea na ukubwa wa banda lako.

Banda lenye ukubwa wa mita 5 x mita 3
(futi 15 x futi 9)
huwatosha kuku sitini (60) wanaotaga,
au kuku 120 wa nyama.

**Vifaa Ndani ya Banda**

Kuku wakiwa wanafugwa
kwa mtindo wa nusu ndani-nusu nje,
au ndani tu,
wanahitaji huduma mbalimbali ndani ya banda.



Banda la kuku wanaofugiwa ndani tu


Vifaa vifuatavyo ni vya muhimu sana katika banda.

**Vilishio**

Hivi ni vifaa vya kuwekea chakula cha kuku.
Ni Muhimu viwe vimetengenezwa vema
ili visiwe chanzo cha upotezaji wa chakula.

Unapotengeneza kilishio
ni lazima ukumbuke kuwa
kuku anatabia ya **kuchakura.**
Husambaza au kupekua pekua chakula kwa miguu
ili apate chakula cha chini.

Tabia hii husababisha
kumwagwa kwa chakula kingi chini.
Hii ni hasara kwako.
Utaidhibiti tu tabia hii
kama utatengeneza vilishio
visivyomwezesha kuku kuchakura.



Kilishio kinachomzuia kuku asimwage chakula


Kilishio hiki unaweza kujitengenezea wewe mwenyewe au anaweza kutengeneza fundi seremala wa hapo kijijini.
Inafaa kilishio kiwe chembamba ili kuku wasiweze kuingia ndani yake.
Pia kiwe kirefu ili kuku wengi waweze kula bila kusongamana.

**Vinywesheo**

Vinywesheo ni vifaa vya kuwekea maji kwa ajili ya kunywa kuku.

Kuna njia nyingi za kutengeneza vinywesheo.
Aina moja ya kinywesheo inayofaa ni kutumia debe.
Kata nafasi ya kunyweshea katika pande zote nne, kama kielelezo kinavyoonyesha.


Kinywesheo
Kilichotengenezwa
kutokana
na debe.



Ili kuepuka msongamano wa kuku wakati wa kunywa maji tengeneza vinywesheo vya kutosha idadi ya kuku ulio nao.

**Makasha ya Kutagia Mayai**

Weka idadi ya makasha ya kutagia mayai inayotosheleza kuku ulio nao.
Makasha yawekwe upande wenye giza kiasi ili kuku wasiogope kuingia na kutaga ndani yake.



Kuku akiwa ndani ya kasha la kutagia mayai

**Usafi Ndani ya Banda**

Geuza takataka za mbao sakafuni mara kwa mara,
ili kuharakisha kukauka kwa kinyesi cha kuku
na unyevu utokanao na maji yanayomwagika.

Takataka zikichafuka badilisha.
Ondoa zile za zamani, weka mpya.
Okota manyoya yote yanayoonekana yakizagaa sakafuni.
Wakati mwingine kuku hula manyoya hayo,
na hivyo kuhatarisha afya zao.

**Kuokota Mayai**

Usiyaache mayai ndani ya makasha ya kutagia,
au sakafuni, kwa muda mrefu.
Okota mayai mara kwa mara,
ili kuepuka kuharibiwa kwa mayai hayo
na kuku wenyewe.

Kuku huwa na tabia ya kula mayai
kama kuna upungufu wa protini
katika chakula unachowapa.

Pia kiasi cha mwanga unaoingia ndani ya banda kikizidi,
kuku hushambulia mayai
au kudonoana wenyewe kwa wenyewe.
Ukiona dalili hizi katika kundi lako,
punguza kiasi cha mwanga
kwa kuziba sehemu za madirisha
kwa vipande vya magunia
au vipande vya makasha ya karatasi ngumu.

Wape kuku majani mabichi ya kutosha mara kwa mara
ili wawe wanakula hayo badala ya kudonoana.
Kama kuku watendelea kula mayai au kudonoana
omba msaada wa mtaalam wa mifugo awakate midomo.

## Njia Nzuri ya Kumbeba Kuku

Watu wengi wanapombeba kuku
wamezoea kumshika miguu,
na kuning'iniza kichwa chini.

Kuku anapobebwa kwa njia hii
hupata shida ya kupumua.
Ingawa hawezi kufa mara moja,
lakini kama unamsafirisha mbali
ataathirika kwa namna fulani.

Kwa mfano atapatwa na kuzunguzungu
kwa sababu mwelekeo wa mzunguko wa damu
unakuwa siyo ule wa kawaida,
yaani anapokuwa wima.
Mbebe kuku kama kinavyoonyesha
kielelezo cha pili ukurasa unaofuata.

Kumbeba au **kumsafirisha kuku** kwa njia nzuri
ni kanuni mojawapo ya ufugaji bora wa kuku.
Unaposafirisha kuku wengi kwa mara moja
tumia chombo chenye nafasi
ya kuwatosha kuku ulio nao.

Kwa mfano tenga la mianzi au matete
hukuwezesha kuwasafirisha kuku
wakiwa wamesimama wima.

Unapomsafirisha kuku mmoja tu,
basi mbebe kwa uangalifu
ili abaki wima
kama kielelezo cha pili kinavyoonyesha.



Njia mbaya ya kumbeba kuku



Njia nzuri ya kumbeba kuku

Katika sehemu hii ya kijitabu,
umejifunza juu ya sifa za banda bora
na njia mbili za kufuga kuku:
Kufuga nusu ndani - nusu nje,
na kufuga ndani ya banda tu.

Umejifunza pia
juu ya hali ya banda inavyotakiwa kuwa,
vifaa vinavyohitajika kuwepo ndani ya banda,
usafi ndani ya banda,
umuhimu wa kuokota mayai mara kwa mara,
na njia nzuri ya kumbeba kuku wakati unamsafirisha.

Katika sehemu ya kijitabu inayofuata
utajifunza juu ya magonjwa ya kuku

## Sehemu ya Nne

# MAGONJWA YA KUKU

## Dalili na Jinsi ya Kudhibiti

Magonjwa ya kuku yapo mengi.
Hata hivyo siyo yote
yanatokea mara kwa mara hapa Tanzania.
Ili uweze kudhibiti
yale yanayotokea katika kundi lako
unahitaji kufahamu
dalili za jumla za magonjwa hayo.

Unapoigundua moja au zaidi
ya dalili za ugonjwa au wadudu
chukua hatua mara moja.
Yapo magonjwa
ambayo yanaweza kuangamiza kundi lote la kuku
katika muda mfupi.

Jihadhari na uwezekano
wa kupatwa na hasara zinazoletwa na magonjwa
ambayo unaweza kuyazuia.

Katika sehemu hii ya kijitabu
utajifunza kwa muhtasari tu
dalili za jumla za magonjwa ya kuku
na jinsi ya kuyadhibiti.

### Dalili za Jumla za Magonjwa ya Kuku

- Kuku kupoteza hamu ya kula.
- Kuzubaa na kukaa mahali pamoja kwa muda mrefu. (Kutochangamka).
- Kushuka kwa kiwango cha utagaji wa mayai.
- Vifaranga kutokua upesi au kudumaa.
- Macho kuwa na rangi nyekundu.
- Kujikunja shingo.
- Kutetemeka, kutoa majimaji puani, mdomoni na machoni.
- Kutoa mharo (kinyesi) wa rangi ya kijani au wenye mchanganyiko na damu.
- Kukonda.
- Kukohoa

Ukiona moja au zaidi
ya dalili hizi katika kundi lako
omba msaada wa mganga wa mifugo
ili achunguze mara moja
na kukushauri jambo la kufanya.

# Muhtasari wa Magonjwa Muhimu ya Kuku na Jinsi ya Kuyadhibiti

| Jina la Ugonjwa | Chanzo | Dalili | Kudhibiti |
|---|---|---|---|
| 1. Kideri (*Newcastle*) | Virusi | Kukohoa, kupumua kwa shida. Mwili kukosa nguvu, shingo kujikunja. | Vifaranga wachanjwe katika juma lao la kwanza. Chanjo la pili wanapofikisha umri wa miezi 4½ (Wanapoanza kutaga) |
| 2. Mdondo (*Coccidiosis*) | Bakteria | Kuhara damu. Kuku hujikusanya pamoja. Hawachangamki. Hushusha mbawa. | Tunza usafi katika banda. Lisha vifaranga chakula kilichochanganywa na dawa *coccidiostat*; na maji yaliyochanganywa na *Amprol*. |
| 3. Ndui ya kuku (*Fowl pox*) | Virusi | Malengelenge kwenye kishungi, na kope za macho. | Kuchanja kuku wote ambao hawajaambukizwa. Watenge kuku wote walioambukizwa. |
| 4. Kikohozi cha kuambukiza (infectious *bronchitis*) | Virusi | Kupumua kwa shida. Kukohoa, utagaji kushuka kwa kiwango cha juu. | Kuchanja kuku wote kabla hawajaambukizwa. |



Kuku mwenye kideri



Kuku mwenye mdondo



Kuku mwenye ndui

# Muhtasari wa Wadudu Muhimu Wanaoshambulia Kuku

Zipo aina tatu za wadudu wanaomshambulia kuku.
Hawa ni **viroboto, papasi** na **utitiri.**
ambao hushambulia kwa nje;
na **minyoo** ambao hushambulia tumboni.
Wote hawa husababisha
kushuka kwa viwango vya utagaji mayai
wa kuku wako.

**Ni muhimu ujue jinsi ya kuwadhibiti wadudu hawa.**

| Jina la Mdudu | Chanzo | Dalili | Kudhibiti |
|---|---|---|---|
| Viroboto | Uchafu, hasa vumbi ndani ya banda la kuku. Viroboto hujificha na kuazaliana katika vumbi. | Wadudu weusi huonekana wanamshambulia kuku kwenye kishungi, kichwani, na uso kwa ujumla. | Tunza usafi wa banda. Nyunyizia dawa za kuuaa wadudu katika banda. Kwa mfano *Doom powder* au *sevin*. |
| Papasi na **utitiri** | - do - | Wadudu wadogo wengi husambaa katika mwili mzima wa kuku. Hunyonya damu. | - do- |
| Minyoo | Kuku kula chakula kilichochafuliwa na kinyesi chao. | Kuku hukonda, hawanawiri. | Dhibiti usafi wa vyakula, maji na vyombo vyake. |

Katika sehemu hii umejifunza:

dalili za jumla za magonjwa ya kuku,
magonjwa manne muhimu ya kuku
hapa nchini,
chanzo na dalili za kila ugonwa,
na jinsi ya kudhibiti kila ugonjwa.

Pia umejifunza

aina mbili za wadudu
wanaomshambulia kuku,
kwa nje na kwa ndani;
chanzo, dalili
na jinsi ya kumdhibiti kila mdudu
tuliyemtaja katika sehemu hii

## Sehemu ya Tano

# KUSIMAMIA UFUGAJI WAKO

## Kutunza Kumbukumbu za Ufugaji wa Kuku

Ili ufanikiwe katika ufugaji wa kuku,
ni jambo muhimu sana kulifahamu vema
kundi la kuku wako.
Ukilifahamu vema kundi lako utaweza:

- Kuchagua kuku bora wa kuzalishia
  kwa kuangalia ubora wa wazazi wao.

- Kufahamu historia ya afya ya kundi,
  kwa mfano
  - umri ambapo vifaranga vilipata chanjo,
  - ni chanjo ya aina gani,
  - magonjwa ambayo yamewahi kushambulia kundi,
  - na dawa ulizotumia katika matibabu.

- Idadi ya kuku wanaokufa.

- Kukadiria kiasi cha chakula ambacho
  kuku wako watahitaji kwa muda fulani
  na aina ya chakula.

- Kujua kila siku kuku wametaga mayai mangapi.

- Kujua utahitaji muda gani
  kutunza kuku wa nyama
  toka vifaranga
  mpaka wanapofikia uzito wa kuchinjwa
  au kuuzwa.

Kadhalika na kuku wa mayai
tangu vifaranga mpaka kutaga.

**Ili uweze kufahamu mambo haya yote unahitaji kutunza kumbukumbu.**

Daftari moja ya kawaida
inatosha kutunzia kumbukumbu
za mambo yote yanayohusu kundi.

Ufuataо hapa chini
ni mfano rahisi wa kutunza kumbukumbu
za kuku wa nyama
tangu wangali vifaranga
mpaka wanapofikia uzito wa kuchinjwa au kuuzwa.

**Kumbukumbu za Kuku wa Nyama**

| | **Tarehe** | **Magonjwa** | **Tiba** |
|---|---|---|---|
| Ukoo wa kuku/aina ............<br>Tarehe ya kuanguliwa ..........<br>Walikonunuliwa .................<br>Idadi yao ............................ | 3.7.92<br>5.9 92 | coccidiosis<br>mdondo | teramycin<br>furazolidone |
| Vyakula Walivyotumia: | **Tarehe** | **Chanjo au Kudhibiti Vimelea na Wadudu** | |
| Chakula mchanganyiko<br>kwa vifaranga: kilo ........<br>**Kwa siku ..........................**<br>kwa wanaokua: kilo........<br>**Kwa siku ..........................**<br><br>Tarehe ya kuuzwa .............<br>Idadi iliyouzwa ...................<br>Umri wa kuku ....................<br>Idadi ya vifo ...................... | 6.8.92<br><br><br>5.10.92 | Amprol katika maji, kinga dhidi ya coccidiosis.<br><br>Kunyunyiza doom powder au sevin powder katika banda-viroboto. | |

**Tenganisha habari hizi katika kurasa tofauti**

## Mfano wa Kumbukumbu Rahisi za Kuku wa Mayai

| Ukoo/Aina ya Kuku ............................................<br>Idadi Ya Kuku Wanaotaga ..................................<br>Idadi ya Makundi ................................................ | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Tarehe | Idadi ya kuku wanaotaga | Kiasi cha Chakula Walichopewa (kilo)/siku | Idadi ya Mayai Waliotaga/siku | Kuku Walio Kufa au Kuondolewa | Taarifa Nyingine |
| | | | | | |

# Jinsi ya Kufahamu Faida Unayopata

Ili uweze kufahamu faida unayopata
kutokana na ufugaji wa kuku
inakupasa kutunza kumbukumbu
za **matumizi** na **mapato** ya kila siku

Kwa mfano
upande wa **matumizi** ingiza

- gharama ya kununua vifaranga
(kama walitotolewa hapo hapo nyumbani
inafaa ukadirie gharama hiyo);

- gharama ya chakula
(kama unatengeneza na kuchanganya
wewe mwenyewe kadiria) kwa kutumia bei za
viungo ghafi.

- gharama ya mafuta ya taa (kama uliwakuza vifaranga kwa joto la taa);
- gharama ya vifaa vya kusafishia banda;
- gharama za madawa ya kinga (chanjo) na tiba;

Upande wa **mapato** ingiza
- mauzo ya mayai;
- mauzo ya kuku hai wasiotaga kutokana na kasoro au uzee;
- gharama ya mayai yaliyotumiwa nyumbani;
- gharama ya mayai yaliyovunjika na hukuyatumia;
- mauzo ya mbolea kutoka katika banda.

Ufuatao ni mfano unaokuonyesha jinsi ya kuingiza taarifa hizi katika daftari yako ya kumbukumbu.

**Kumbukumbu za Matumizi na Mapato**

| Matumizi | Shs. | Mapato | Shs. |
|---|---|---|---|
| Kununua vifaranga 20 (@50/=) | 1,000/= | Mauzo ya mayai 80 (@30/=) | 2,400/= |
| Kununua dagaa (kilo 5) | 1,500/= | | |
| Kununua mashudu (kilo 3) | 300/= | Mauzo ya mbolea madebe 4 (@200/=) | 800/= |
| Kununua chumvi (kopo 1) | 100/= | | |
| Chanjo vifaranga 20 (@ 5/=)n.k. | 100/= | | |
| | | Mayai yaliyotumiwa nyumbani 20 | 600/= |

Kila mwisho wa mwezi jumlisha hesabu ya kila upande. Ili ufahamu faida uliyopata, fanya hesabu:

**Mapato Yote - Matumizi Yote = Faida**

Kama ni kuku wa nyama fanya hesabu hii baada ya kuuza kuku wote.

# Neno la Mwisho

Katika kijitabu hiki
umejifunza aina za kuku na koo zake.
Pia umejifunza
jinsi ya kuboresha kuku wa kienyeji
kwa kutumia jogoo bora.
Umejifunza sifa za banda bora la kuku,
na njia mbili za kufuga kuku ili unufaike.

Pamoja na hayo yote
umejifunza lishe ya kuku
kutumia vyakula ambavyo
vinapatikana katika mazingira yako,
hapo kijijini.

Tena unaweza kuvichanganya wewe mwenyewe
ukifuata kwa uangalifu
vipimo tulivyotoa,
ili upate milo kamili ya kuku wako.

Kwa ujumla tumeandika kijitabu hiki
tukilenga kukusaidia wewe mkulima mdogo
ambaye unafuga kuku wa kienyeji.

Tulichofanya ni kupendekeza
mbinu mbali mbali za kustawisha ufugaji wako.
Mbinu zote hizi zinaweza kutekelezwa kwa vitendo;
tena kwa gharama nafuu.
Zitatoa matokeo mazuri
kama utazitekeleza kwa usahihi.

Hata hivyo huwezi kutekeleza
mbinu zote hizi kwa mara moja.
Hili ni changamoto kwako.

Chagua kwa uangalifu
mtindo wa ufugaji unaokufaa,
halafu anza kutekeleza jambo moja moja
kati ya yale yanayowezekana.

Tunatumaini juhudi utakazofanya
katika kuyatumia maarifa haya kwa vitendo
zitakupatia matokeo ya kimaendeleo kiuchumi.

Kumbuka

**Maarifa**
**bila vitendo**
**hayatakusaidia kitu.**

Kwa ujumla katika kijitabu hiki
umejifunza mbinu zitakazokusaidia
kuboresha kuku wako wa kienyeji,
ili wakupatie mazao yakutosha.

Kijitabu kingine "**Kufuga Kuku wa Biashara**"
kinahusu jinsi ya kufuga kuku wa biashara.
Kuku hao wanaweza kuwa wa mayai au wa nyama.

## Tukumbuke Maneno Haya

**Unalifahamu kila neno lifuatalo?**
**Ikiwa hulifahamu neno**
**angalia katika ukurasa uliotajwa.**

**Amprol**: dawa ya kinga dhidi ya mdondo (coccidiosis) katika vifaranga

**Carotine (karotini)**: viini katika majani mabichi; hufanya kiini cha yai kuwa na rangi ya njano

**Chotara**: kuku waliozalishwa kutokana na koo mbili tofauti

**Coccidiosis au mdondo**: ugonjwa wa kuhara, pengine damu, au mdondoambao hushambulia kuku hasa vifaranga

**Doom powder**: dawa ya unga ya kuua wadudu kama viroboto n.k.

**Furazolidone**: dawa ya unga ya dhidi ya kukinga vifaranga

**Huria**: kufuga kuku bila kuwadhibiti ndani ya zizi

**Kideri**: ugonjwa wa kuhara kinyesi cha rangi mchanganyiko wa nyeupe na njano

**Kitalu**: mahali pa kukuzia vifaranga

**Koo la kuku**: kuku jike lililowahi kutaga

**Kuchakura**: tendo la kuku kuparuza na kupekuapekua chini kwa vidole vya miguu kutafuta chakula

**Luseni**: mmea wa jamii ya mikunde;
majani yake hutumika kulisha mifugo

**Lusina**: mti wa jamii ya mikunde, hurutubisha udongo;
majani yake hutumika kulisha mifugo

**Marejea**: mmea wa jamii ya mikunde; majani yake,
makubwa kuliko luseni, hutumika kulisha mifugo

**Mashudu**: machicha ya alizeti au pamba baada
ya kukamua mafuta

**Serena**: aina ya mtama mfupi, una punje nyekundu

**Temba**: kuku anayekaribia kutaga

**Teramycin**: dawa ya unga kukinga vifaranga
dhidi ya magonjwa

**Ukoo wa kuku**: kuku wenye asili moja

**Viungo ghafi**: vitu mbali mbali (vyakula) vinavyotumika
katika uchanganyaji wa chakula cha
kuku/vifaranga

MKL
SF489
.K8

# Ofisi za INADES - Formation

**Tanzania**
**INADES - Formation, P.O. Box 203,Dodoma, Tanzania**

**Kenya**
**INADES - Formation, P.O. Box 14022,Nairobi, Kenya**

**Ofisi Kuu**
**INADES - Formation 08 B.P. 8 Abidjan, Ivory Coast**

**Burkina - Faso**
**INADES - Formation, B.P 1022, Ouagadougou**

**Burundi**
**INADES - Formation, B.P. 2520, Bujumbura**

**Cameroon**
**INADES - Formation, B.P. 11, Younde**

**Chad**
**INADES - Formation, B.P. 945, N'djamena**

**Ethiopia**
**Agri-Service Ethiopia, P.O. Box 2460, Addis Ababa**

**Ivory Coast**
**INADES - Formation, B.P. 2007, Bouake 01**

**Rwanda**
**INADES - Formation, B.P. 866, Kigali**

**Togo**
**INADES - Formation, B.P. 39, Atakpame**

**Zaire**
**INADES - Formation, B.P. 5717, Kinshasa - Gombe**